# KUCHUNGUZA DHAMIRA ZA MAPENZI NA USALITI KATIKA RIWAYA YA MFADHILI

**FATMA RASHID MOH'D**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUTIMIZA MASHARTI**

**YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI (M.A. KISWAHILI)**

**YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2019**

## ITHIBATI

Aliyeweka saini hapa chini anathibitisha kuwa, ameisoma tasnifu hii yenye mada: ***Kuchunguza Dhamira za Mapenzi na Usaliti katika Riwaya ya Mfadhili*** *na*kupendekeza ikubaliwe na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya kupatiwa Shahada ya Uzamili ya Sayansi jamii katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

.................................................

**Dr. Muhamed Omary Maguo**

(Msimamizi)

Tarehe.........................................

## HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga au kunakili kwa njia yoyote ile, iwe ama kazi nzima au sehemu ya tasnifu hii, kwa ajili ya utafiti, kujisomea au kufanya marejeo ya kitaaluma bila kibali cha maandishi cha Mkuu wa Kurugenzi ya Taaluma za Uzamili, Utafiti na Uchapaji kwa niaba ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

## IKIRARI

Mimi, **Fatma Rashid Moh`d,** nathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu binafsi na kwamba haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au shahada nyingine yoyote.

.......................................

Saini

.......................................

Tarehe

## TABARUKU

Kwa heshima na taadhima, natabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapenzi: Bw. Rashid Mohammed Ali na Bi. Amina Said Ali kwa kunizaa, kunilea na kunisomesha bila ya kuchoka. Pia kwa mume wangu kipenzi Said Omar Said pamoja na watoto wangu wapendwa kwa kunipa moyo. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awasamehe makosa yao na awajaalie wawe miongoni mwa waja wa Peponi kwa rehema na mapenzi yake (Amiin).

## SHUKURANI

Kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu (S.W) kwa kuniumba, binadamu na kunijaalia uzima, afya, uvumilivu, uwezo, busara na hekima kwa kuifanya kazi hii ya utafiti hadi kukamilika. Kwa shukurani fupi nasema: Alhamdulillah Rabbil Alamiin. Namuomba Mwenyezi Mungu anijaalie ziada za kheri.

Pili, shukurani zangu za dhati ziwafikie wazazi wangu wapenzi: kwa juhudi zao za kunizaa, kunilea na kunisomesha bila ya kuchoka hadi nikafikia katika ngazi hii ya elimu. Nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awasamehe makosa yao na awajaalie wawe miongoni mwa wale wataoingia peponi kwa rehema na mapenzi ya Allah (Amiin).

Tatu, Shukrani za pekee zimfikie Msimamizi wangu Dr. Muhamed Omary Maguo, ambaye amenikuza kitaalumma na kushauriana kila hatua hadi tasnifu hii kukamilika. Dr. Muhamed Maguo amekuwa akiisimamia na kufanya kazi hii bila ya kuchoka na kunitia hamasa kubwa niweze kummaliza kazi hii kwa wakati muwafaka. Sina budi kumuombea kwa Allah amlipe malipo mema (Amiin).

Shukurani nyengine ziufikie uongozi mzima wa Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kuanzia makao makuu Dar es Salaam hadi tawi la Pemba. Kwa sababu hawa ni wengi naomba niwataje baadhi; Prof. Emmanuel Mbogo, Dkt. Zelda Elisifa, Dkt. Hilda Pembe, mwalimu Bakari Kombo Bakari, mwalimu Nassor Ali Suleiman, mwalimu Sharifu na wengineo. Hawa wote walinisaidia kwa njia moja ama nyengine hadi kukamilika kwa tasnifu hii.

Mwisho napenda kuishukuru familia yangu. kwa kunishauri, kunitia moyo, busara, juhudi, hamasa na uvumilivu wao mkubwa katika kipindi chote cha masomo hadi sasa kwa pale walipokua hatuko pamoja kwa sababu ya masomo, hakika walitambua kuwa elimu ni ufunguo wa maisha na wala elimu haina mwisho.

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu *Kuchunguza Dhamira za Mapenzi na Usaliti katika Riwaya ya Mfadhili.* Lengo kuu ni kuchunguza dhamira za mapenzi na usaliti katika riwaya ya Mfadhili ya Hussein Tuwa. Utafiti huu umehusisha malengo mahsusi matatu ambayo ni kubainisha dhamira za mapenzi zilizojitokeza katika riwaya ya *Mfadhili*. Lengo la pili ni kubainisha dhamira za usaliti zilizojitokeza katika riwaya ya *Mfadhili* na lengo la tatu ni kubainisha mbinu za kisanaa zilivyoibua dhamira za mapenzi na usaliti katika riwaya ya *Mfadhili*. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Mwitiko wa Msomaji katika lengo la kwanza la kwanza na la pili sambamba na suali la kwanza na la pili na nadharia ya Simiotiki katika lengo la tatu na suala la tatu. Mbinu iliyotumika kukusanyia data ilikuwa ni mbinu ya usomaji makini pamoja na upitiaji wa nyaraka maktabaniambapo mtafiti aliisoma kwa kina riwaya teule huku akidondoa data ambazo hatimae zilijibu maswali ya utafiti huu. Data za utafiti huu zilichambuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo. Aidha, utafiti huu uliongozwa na maswali matatu ya utafiti ambapo swali la kwanza lilikuwa ni; *Ni dhamira zipi za mapenzi zilizojitokeza katika riwaya ya Mfadhili?* Matokeo ya utafiti huu yameonesha kuwa riwaya teule ya *Mfadhili* imeonesha mapenzi ya dhati ambayo ni kati ya baba na mtoto wake wa kambo, mtu na rafiki yake, mapenzi kati ya mtu na mchumba wake, mapenzi katika ndoa, mapenzi kati ya mtu na wifi yake, mapenzi kati ya daktari na jamii na mapenzi ya dhati kati ya mkuu wa kazi na wafanyakazi wake. Kwa upande mwengine kuna mapenzi ya uongo ambayo yamejitokeza kati ya mke na mume wake wa ndoa, mapenzi ya uongo kati ya mtu na mchumba wake na mapenzi ya uongo kati ya marafiki. Swali la pili lililoongoza utafiti huu lilikuwa; *Ni dhamira zipi za usaliti zilizojitokeza katika riwaya ya Mfadhili?* Data za utafiti zilionesha kwamba dhamira ya usaliti imejitokeza katika ndoa, usaliti katika mtu na mchumba wake, usaliti kati ya marafiki na usaliti unaofanywa watumishi wa umma na usaliti unaofanywa na wafanyakazi wa afya. Swali la tatu lililoongoza utafiti huu lilikuwa; *Ni mbinu zipi za kisanaa zinazoibua dhamira za mapenzi na usaliti katika riwaya ya Mfadhili*? Data za utafiti zilionesha kwamba dhamira ya mapenzi na usaliti zimeibulia kupitia vipengele vya lugha, wahusika na mandhari.

## YALIYOMO

ITHIBATI. .......... ii
HAKIMILIKI .......... iii
IKIRARI…… .......... iv
TABARUKU .......... v
SHUKURANI .......... vi
IKISIRI……….. .......... viii
YALIYOMO .......... ix
ORODHA YA MAJEDWALI .......... xv
ORODHA YA VIFUPISHO .......... xvi

**SURA YA KWANZA: UTANGULIZI WA UJUMLA .......... 1**

1.1 Utangulizi .......... 1
1.2 Usuli wa Mada .......... 1
1.3 Tatizo la Utafiti .......... 8
1.4 Malengo ya Utafiti .......... 8
1.4.1 Lengo Kuu .......... 9
1.4.2 Malengo Mahsusi .......... 9
1.4.3 Maswali ya Utafiti .......... 9
1.5 Umuhimu wa Utafiti .......... 9
1.6 Mipaka ya Utafiti .......... 10
1.7 Mpangilio wa Tasnifu .......... 10

**SURA YA PILI: MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA MKABALA WA KINADHARIA ........................................................................................... 12**

2.1 Utangulizi ........................................................................................ 12

2.2 Ufafanuzi wa Istilahi Mbalimbali ........................................................ 12

2.2.1 Maana ya Riwaya ........................................................................... 13

2.2.2 Maana ya Dhamira .......................................................................... 15

2.2.3 Maana ya Mapenzi ........................................................................... 15

2.2.4 Maana ya Usaliti ............................................................................. 16

2.3 Dhana ya Mbinu za Kisanaa ................................................................ 17

2.3.1 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Dhamira ........................................ 19

2.3.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi kuhusu Maandishi ya Hussein Issa Tuwa ..... 22

2.4 Pengo la Utafiti ................................................................................ 27

2.5 Mkabala wa Kinadharia ..................................................................... 27

2.5.1 Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ...................................................... 28

2.5.1.1 Mihimili ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji .................................. 29

2.5.1.2 Mapungufu ya Nadharia ya Mwitiko wa Msomaji ............................... 31

2.5.2 Nadharia ya Simiotiki. ..................................................................... 32

2.5.2.1 Misimbo ya Nadharia ya Simiotiki ................................................... 33

2.6 Hitimisho ......................................................................................... 34

**SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI ........................................................ 35**

3.1 Utangulizi ........................................................................................ 35

3.2 Eneo la Utafiti .................................................................................. 35

3.3 Kundi Lengwa ................................................................................... 36

3.4 Sampuli na Usampulishaji ........................................................................ 36

3.4.1 Usampulishaji Lengwa ............................................................................ 37

3.5 Aina za Data ............................................................................................ 37

3.5.1 Data za Awali .......................................................................................... 37

3.5.2 Data za Upili ........................................................................................... 38

3.6 Mbinu za Ukusanyaji wa Data ................................................................ 38

3.6.1 Mbinu ya Usomaji Makini ...................................................................... 39

3.6.2 Mbinu ya Upitiaji Nyaraka ..................................................................... 39

3.7 Mbinu za Uchambuzi wa Data ................................................................ 40

3.7.1 Mkabala wa Kimaelezo ........................................................................... 40

3.8 Hitimisho ................................................................................................. 40

**SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA UCHAMBUZI WA DATA .................. 41**

1.1 Utangulizi ................................................................................................ 41

4.2 Usuli wa Mwandishi: Hussein Issa Tuwa ............................................. 41

4.3 Muhtasari wa Riwaya ya Mfadhili ......................................................... 43

4.4 Dhamira ya Mapenzi katika Riwaya ya Mfadhili .................................. 44

4.4.1 Mapenzi ya Dhati .................................................................................... 45

4.4.1.1 Mapenzi ya Kweli katika Ndoa aliyoonesha Gaddi Bullah kwa Nyambuja ........................................................................................... 45

4.4.1.2 Mapenzi ya Dhati kati ya Marafiki aliyokuwanayo Nunu kwa Dania..... 47

4.4.1.3 Mapenzi ya Dhati ya Mtoto na Wazazi wake Waliyonayo Wazazi wake Dania ............................................................................... 49

4.4.1.4 Mapenzi ya Dhati kati ya Mtu na Mtoto; Dania na Junior ...................... 50

4.4.1.5 Mapenzi ya Dhati ya Baba na Mtoto Wake wa Kambo; Aliyoonesha Gaddi Bullah kwa Junior ........ 52
4.4.1.6 Mapenzi ya Dhati kati ya Mtu na Wifi Yake kama alivyoyaonesha Bi. Hanuna kwa Dania ........ 53
4.4.1.7 Mapenzi ya Dhati kati ya Mtu na Rafiki yake Aliyonayo Nunu kwa Dania ........ 55
4.4.1.8 Mapenzi ya Dhati ya Mtu na Mchumba Wake kama alivyoyaonesha Gaddi Bullah kwa Dania ........ 56
4.4.1.9 Mapenzi ya Dhati kati ya Mkuu wa Kazi na Wafanyakazi wake Aliyonayo Mama Mlole ........ 59
4.4.1.10 Mapenzi ya Dhati kati ya Daktari na Jamii. ........ 62
4.4.2 Mapenzi ya Uongo ........ 64
4.4.2.1 Mapenzi ya Uongo katika Ndoa Aliyonayo Nyambuja kwa Gaddi Bullah ........ 64
4.4.2.2 Mapenzi ya Uongo kati ya Mtu na Mchumba wake Aliyonayo Jerry kwa Dania ........ 65
4.4.2.3 Mapenzi ya Uongo ya Mtu na Mchumba wake kama Alivyoyaonesha Dania kwa Gaddi Bullah ........ 67
4.5 Dhamira ya Usaliti katika Riwaya ya Mfadhili ........ 69
4.5.1 Usaliti wa Mtu na Mchumba wake ulivyofanywa na Jerry Dhidi ya Dania ........ 69
4.5.2 Usaliti wa Mtu na Mchumba wake Unaofanywa na Dania kwa Gaddi Bullah ........ 71

4.5.3 Usaliti wa Wahudumu wa Afya kama Ulivyofanywa na Dokta Virani kwa Gaddi Bullah ........ 73

4.5.4 Usaliti wa Mtu na Wifi yake kama Ulivyofanywa na Nunu kwa Bi Hanuna ........ 75

4.5.5 Usaliti wa Wajane kama Aliofanyiwa Bi Hanuna na Shemegi zake ....... 76

4.5.6 Usaliti wa Wanandoa Alioufanya Nyambuja Dhidi ya Gaddi Bullah ..... 78

4.5.7 Usaliti Anaofanyiwa Gaddi Bullah na Wafanyakazi ........ 80

4.6 Mbinu za Kisanaa Zinazoibua Mapenzi na Usaliti katika Riwaya ya Mfadhili........ 82

4.6.1 Lugha Inavyoibua Dhamira ya Mapenzi na Usaliti katika Mfadhili ....... 82

4.6.1.1 Nahau ........ 83

4.6.1.2 Misemo ........ 84

4.6.1. Methali ........ 87

4.6.1.4 Tashbiha........ 88

4.6.1.5 Tashhisi ........ 90

4.6.1.6 Kuchanganya Ndimi ........ 92

4.6.1.7 Takriri ........ 93

4.6.2 Mandhari Yanavyoibua Dhamira ya Mapenzi na Usaliti katika Mfadhili........ 95

4.6.2.1 Mandhari ya Oysterbay........ 96

4.6.2.2 Mandhari ya Ofisini kwa Gaddi Bullah ........ 97

4.6.3 Wahusika Wanavyoibua Dhamira ya Mapenzi na Usaliti ........ 99

4.6.3.1 Gaddi Majid Bullah........ 99

4.6.3.2 Dania ........ 100

4.6.3.3 Bi. Hanuna ........ 101

4.6.3.4 Mama Mlole ........ 103

4.6.3.5 Nyambuja Mollel ........ 104

4.6.3.6 Nunu ........ 105

4.6.3.7 Jerry Gwandume ........ 107

4.6.3.8 Dokta Virani ........ 107

4.7 Hitimisho ........ 108

**SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 110**

5.1 Muhtasari wa Tasnifu ........ 110

5.2 Matokeo ya Utafiti ........ 112

5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza ........ 113

5.2.2 Lengo Mahususi la Pili ........ 113

5.2.3 Lengo Mahususi la Tatu ........ 113

5.3 Hitimisho ........ 114

5.4 Mapendekezo ........ 114

5.4.1 Mapendekezo kwa Watafiti Wengine ........ 114

5.4.2 Mapendekezo kwa Taifa ........ 115

5.4.3 Mapendekezo kwa Jamii ........ 115

**MAREJELEO ........ 116**

## ORODHA YA MAJEDWALI

Jadwali Na. 1 Dhamira ya Mapenzi ya Dhati katika *Mfadhili*.................................. 63

Jadwali Na. 2 Dhamira ya Mapenzi ya Uongo katika *Mfadhili*................................ 68

Jadwali Na. 3 Dhamira ya usaliti katika *Mfadhili*..................................................... 81

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| Bi. | Bibi |
| Bw. | Bwana |
| Dkt | Daktari |
| Dr | Doctor |
| M.A | Master of Art |
| OUT | Open University of Tanzania |
| Prof | Profesa |
| SUZA | State University of Zanzibar |
| S. W | Subhanahu Wataalah |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| Uk. | Ukurasa |
| Ltd | Limited |
| Ed | Edition |
| Na | Namba |
| TTCL | Tanzania Telecommunication Company Ltd. |
| A.S | Alayhi Salaam |
| S.A.W | Salallahu Alayhi Wasalaam |

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA UJUMLA

## 1.1 Utangulizi

Sura hii kimsingi imeshikamana na vipengele muhimu vya awali vya kiutafiti ambavyo mtafiti alivifafanua. Vipengele hivyo ni pamoja na usuli wa mada, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mpangilio wa tasnifu na hitimisho.

## 1.2 Usuli wa Mada

Mapenzi na usaliti yameanza tokea kuumbwa kwa binadamu katika uso wa dunia. Vitabu vitukufu ambavyo ni Qur-ani na Biblia vinaeleza kuwa kifo cha kwanza cha binadamu kilitokana na mapenzi na usaliti. Vitabu vinasimulia kuwa bibi Hawa, mke wa Nabii Adamu alizaa watoto wawili wawili (mapacha), mwanamke na mwanamme kwa kila mimba. Kila mwanamme alitakiwa kuoa ndugu wa kike wa mwenziwe. Hivyo kila mmoja alipangiwa mke kwa mujibu wa sheria za wakati huo. Mtoto mmoja wa kiume alikataa kumuoa mwanamke aliyepangiwa kwa sababu yeye alikuwa amempenda ndugu yake na kutaka kumuoa, hivyo ili kutatua hili Mwenyezi Mungu akawataka ndugu hao watoke nje ya mji na sadaka zao na yule ambaye sadaka yake itakubaliwa atamuoa mwanamke huyo. Walipotowa sadaka hizo mwanamme ambaye alipangiwa mwanamke yule wa mwanzo ndie aliyekubaliwa sadaka yake. Kuona hivyo mwanamme yule ambaye haikukubaliwa sadaka yake alimsaliti ndugu yake na kumuua hapo hapo. Katika Qur-ani tukufu kisa hiki kinasimulia kama ifuatavyo:-

> "Na wasomee habari za wana wawili wa Adam kwa kweli. Walipotowa mhanga, ukakubaliwa wa mmoja wao, na wa mwengine haukukubaliwa. Akasema: nitakuua. Akasema mwengine: Mwenyezi Mungu huwapokelea wachamungu. Ukininyooshea mkono wako kuniua, mimi sitakunyooshea mkono wangu kukuua. Hakika mimi namuogopa Mwenyezi Mungu, Mola wa walimwengu wote. Mimi nataka ubebe dhambi zangu na dhambi zako, kwani wewe utakuwa miongoni mwa watu wa motoni. Na hayo ndiyo malipo ya wenye kudhulumu. Basi nafsi yake ikampelekea kumuua nduguye, akamuua na akawa ni miongoni mwa wenye kukhasirika. Hapo Mwenyezi Mungu akamleta kunguru anayefukua katika ardhi ili amwonyeshe vipi kumsitiri nduguye, akasema Ole wangu! Nimeshindwa kuwa kama kunguru huyu nikamsitiri ndugu yangu? Basi akawa ni miongoni mwa wenye kujuta. (5:27- 31).

Aidha aya hizi zimetolewa ufafanuzi na Mtume (S.A.W) katika tafsiri ya Quran tukufu. Mfasiri Ibnu Kathiri akinakili hadithi ya Mtume (S.A.W) iliyosimuliwa na Abdalla bin Massuud kuwa:

> "Alikuwa Adam (AS) hazai mtoto wa kiume ila pamoja nae huzaa mtoto wa kike, sasa ikawa mtoto wa kike anayezaliwa upande mmoja humuozesha mtoto wa kiume wa upande wa pili. Miongoni mwa watoto wa kiume wa nabii Adamu (AS) ni Haabil na Kaabil na kila mmoja alikuwa na mdogo wake wa kike. Kaabil alikuwa mkulima na Haabil alikuwa mfugaji. Kaabil ndie aliyekuwa mkubwa na ndugu yake wa kike alikuwa mzuri sana kuliko ndugu wa Haabil. Haabil akataka kumuoa ndugu wa Kaabil lakini Kaabil akakataa na akasema: "Huyu amezaliwa na pamoja na mimi kwahiyo nina haki zaidi ya kumuoa". Lakini baba yao akaamuru kuwa Haabil ndie aliye na haki ya kumuoa, jambo hilo likamkasirisha Kaabil. Haabil na Kaabil wakaenda kutowa sadaka Jangwani, ili yule sadaka yake itahayokubaliwa na Mwenyezi Mungu ndiye ambaye atakuwa na haki ya kumuoa ndugu wa Kaabil. Walipotowa sadaka zao, sadaka ya Haabil ilikubaliwa na ya Kaabil ikawachwa, Kaabil akakasirika na akamwambia ndugu yake "Nitakuua ili usimuoe ndugu yangu." Haabil akamjibu kaka yake "Hakika aliyeikubali sadaka ni Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu anakubali sadaka ya yule amchae." Kutokana na hilo Kaabil akamuua ndugu yake Haabil na kumfukia kwenye ardhi.

Aidha katika Bibilia takatifu Agano la kale, kisa kama hicho kinaelezewa katika kitabu cha mwanzo 4:1-11 kama ifuatavyo:

> 1.“Adam akamjuwa mkewe, naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema “Nimempata mtoto mwanamume kwa bwana. 2. Akaongeza akamzaa nduguye, Habil. Habil alikuwa mchunga kondoo na Kaini alikuwa mkulima ardhi. 3. Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa Bwana. 4. Habil naye akaleta mazao kwanza kwa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. Bwana akamtakabali Habil pamoja na sadaka yake. 5.Bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhibika sana uso wake ukakunjamana. 6. Bwana akamwambia Kaini, kwa nini unaghadhabu? Na kwanini uso wako umekunjamana? 7. Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, imekuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde. 8. Kaini akamwambiya Habil nduguye (twende uwandani). Ikawa walipokuwepo uwandani, Kaini akamwinukia nduguye, akamuua. 9. Bwana akamwambia Kaini, yuko wapi Habil ndugu yako? Akasema sijuwi, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu? 10. Akasema umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako zinalilia kutoka katika ardhi. 11. Basi sasa umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kichwa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako.”

Aidha dhana kuhusu mapenzi imekuwa na mitazamo mbalimbali kwa kuwa mapenzi si dhana iliyosawa kwa watu wote, mahala (sehemu) zote au nyakati zote. Kwa mfano kuna aina mbalimbali za mahusiano ambayo tunaweza kusema ni mapenzi kama vile mapenzi baina ya mzazi na mtoto wake, dada na kaka, urafiki au mapenzi ya ngono. Pamoja na hayo kila aina ya penzi au uhusiano unaweza ukachukua aina tofauti ya mfumo.

Njia pekee ambayo tunaweza kuyafahamu mapenzi ni kupitia lugha ya mapenzi ambayo hutumika kubeba jukumu zito la kuelezea nini kilichomo ndani ya mapenzi. Kwa sababu lugha hutumiwa na wanaume na wanawake katika kujieleza na kusikilizana (Rhees 1969).

Miongoni mwa wataalamu waliojadili dhana ya mapenzi ni Setiya (2014)akimrejelea Velleman (1999) ambaye anaeleza kuwa mapenzi ni maamuzi, akionyesha kuwa si

kitu chenye kuruhusika lakini pia si kitu kinachohitajika. Wakati alipouliza kwa nini tunawapenda baadhi ya watu na watu wengine hatuwapendi, hakuweza kutoa sababu, lakini hii ni kutokana na tofauti muhimu za kihisia na upeo wa nguvu za kimaono.

Perlman (2013) katika mada anayoiita *The Emerging Syntheisis of love as a feeling and love as Intention*, ameeleza mapenzi katika mitazamo miwili ambayo ni mapenzi kama hisia na mapenzi kama kusudio (dhamira). Mapenzi yanaweza kuwa ni hisia zinazoelezewa kutokana na ukweli kwamba yanakuwa yanajengwa na mambo matatu, kwanza yanakuwa na ushawishi ambao huthibitishwa na mazingira ya nje na huwa ni yenye kujionesha wazi wazi. Pili hutawaliwa na mambo ya nje ambayo ni nguvu za kimaono ambazo ziko nje ya udhibiti wa binaadamu. Na mwisho mapenzi kama hisia kwa kawaida huwa sehemu kuu au matamshi ambayo ni makubwa kuliko matamshi ya kifo *(mortal will).* (Tafsiri ni ya mtafiti wa kazi hii).

Perlman (ameshatajwa) akiendelea kueleza mapenzi kama dhamira anasema kuwamapenzi huwa yako katikauhalisia wa kimaumbile, yanajitegemea yenyewe na yako wazi. Aidha mapenzi hujumuisha matashi ambayo ni yenye nguvu na uwezo mkubwa kutafsiriwa katika matendo. Kwa sababu aina hii ya mapenzi yanaota kutokana na matashi ya mtu binafsi. Kimaumbile mapenzi ni yenye kujitegemea (hayategemei sifa na muonekano wa nje). Perlman (ameshatajwa) akimrejelea Pack (1978) ameelezea aina hii ya mapenzi kama dhamira, pale alipotafsiri kuwa mapenzi ni tendo la kimatashi (kidhamira) ambayo huitwa dhamira na vitendo na pia hudhihirisha chaguo. Mapenzi kama dhamira kwa kawaida hujengwa na sehemu ya mawazo ya kidini na kisiasa ambayo yanalingania kutokuwepo nguvu na kusameheana.

Pia, Fitness (2001) aliwarejelea Jones and Burdette (1994) wanaona kuwa usaliti ni uharibifu wa hali yajuu unaoharibu mahusiano mazuri yaliyopo ambayo wenza walishayawekezea rasilimali nyingi zikiwemo vitu hata maono. Fitness, (ameshatajwa), akiwarejelea Cosmides and Tooby (1992) wanaeleza kuwa binaadamu hufikiwa na aina kadhaa za usaliti katika aina tofauti za mahusiano.Kwa mfano usaliti bainaya wenza (wanandoa), marafiki au kikundi cha watu. Kwa kawaida watu hufikiria kuwa usaliti hutokea katika mapenzi tu, hii ni kwa sababu mara nyingimaandiko huonesha zaidi usaliti baina ya mahusiano ya wenza (wanandoa) au wapenzi kama walivyofanya hivyo Hansson, Jones and Fletcher (1990) Jones and Burdette (1994). Hata hivyo Shackelfod na Buss (1996) wanadai kuufahamu zaidi usaliti na wanaona ni muhimu sana kuzingatia aina ya mahusiano ambayo ndani yake usaliti unatokezea kwa sababu kila aina ya uhusiano inakuwa na matarajio yake.

French na wenzake (2009) wanaeleza kuwa usaliti unaweza kuwa ni shambulio lenye kuathiri kutokana na kuwa linapiga na kuathiri mawazo ya ndani kabisa ya mtu na kumuacha akiwa ameathirika mno. Pia humfanya awe na hasira na kutamka maneno kwa vile hushughulikiwa tofauti na matarajio au kudanganya au kuvunjiwa heshima.

Aidha, Salim (2015) ambae ametafiti mada inayohusuKuchunguza ufasihi simulizi unaojitokeza ndani ya hadithi za *Kusadikika* na *Adili na Nduguze*. Katika utafiti huo amechambua dhamira ya mapenzi ambapo ameeleza kuwa mapenzi yana ncha mbili ambazo ni mapenzi ya kweli na mapenzi ya uongo. Anaendelea kueleza kuwa mapenzi ya kweli ni yale ambayo mwenye mapenzi huwa yuko tayari kutoa chake bila ya kujali na kumpa anayempenda.